

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Telegrams “REGCOM” Shinyanga
Simu Na: 028 – 2762222
Fax Na: - 2762310
Barua pepe: ras.shinyanga@tamisemi.go.tz
ras@shinyanga.go.tz
Tovuti: www.shinyanga.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S. L. P 320,
Shinyanga

TAARIFA KWA VYOMBO VY A HABARI

**YAH: ZIARA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA
MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA MKOANI SHINYANGA
TAREHE 07 – 11 JULAI, 2018**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), atafanya ziara ya kikazi Mkoani Shinyanga kuanzia tarehe 07 – 11 Julai, 2018, katika Halmashauri zote sita (6) za Mkoa wetu.

Lengo la ziara hii ni kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za maendeleo pamoja na kukagua masoko ya pamba.

Pamoja na shughuli hizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu atazungumza na wananchi na watumishi wa Umma kwa kila Halmashauri.

Aidha, tarehe 10 Julai, 2018 Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa mpango wa Bima ya Afya kwa wakulima kupitia vyama vya Ushirika ambao Kitaifa utafanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Wilayani Kahama.

Wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga mnaombwa kujitokeza kwa wingi kumpokea Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapopita katika maeneo yenu.

Zainab R. Telack,
Mkuu wa **Mkoa,**
Shinyanga
05/07/2018